# MUONGOZO WA MAFUNZO YA UJUMUISHAJI WA MASUALA YA KIJINSIA KWA WAKULIMA WA KILIMO HAI



## Juni 2020

Achieving gender equality requires the engagement
of women and men, girls and boys.
It is everyone's responsibility

Ban Ki-moon

# MUONGOZO WA MAFUNZO YA UJUMUISHAJI WA MASUALA YA KIJINSIA KWA WAKULIMA WA KILIMO HAI

## Juni 2020

Achieving gender equality requires the engagement
of women and men, girls and boys.
It is everyone's responsibility

Ban Ki-moon



## YALIYOMO:

**1.0 UTANGULIZI** **7**
1.2 Walengwa 7
1.3 Mbinu ya ufundishaji 8

**2.0 MUUNDO WA MUONGOZO** **9**

**3.0 KUANDAA MAFUNZO YAKO** **12**

**4.0 MBINU KWA MUWEZESHAJI** **13**

**5.0 VIAMBATANISHO MUHIMU** **14**
5.1 Kiambatanisho I: Muhtasari wa pendekezo la mafunzo 14
5.2 Kiambatanisho II: Ajenda ya muwezeshaji 16
5.3 Kiambatanisho III: Programu ya mafunzo 18
5.4 Kiambatanisho IV: Zana ya uchambuzi wa jinsia, uwezo wa kufikia na kudhibiti rasilimali kwa ngazi ya familia na siasa. 19
5.5 Kiambatanisho V: Tathimini ya mahitaji ya kijinsia ya msingi 20
5.6 Kiambatanisho VI: Masuala ya jinsia na mfumo wa kimkakati. 21
5.7 Kiambatanisho VII: Muongozo wa tathimini na maswali baada ya mafunzo. 21
5.8 Kiambanisho VIII: mbinu za kuunda makundi 23
5.9 Kiambatanisho IX: Mpangilio na vifaa 23

## KUHUSU MUONGOZO

Muongozo huu unalenga wafanyakazi wa taasisi na wawezeshaji wan je na wa ndani ambao watapeleka elimu ya masuala ya kijinsia kwa vikundi vya mafunzo vya familia za wakulima vilivyopo na vipya. Wawezeshaji hawa wa vikundi vya familia za wakulima watajengewa uwezo wa masuala ya kijinsia kupitia mafunzo yatakayofanya na taasisi ya Kilimo hai Tanzania (TOAM) na kupeleka elimu hiyo kwa wakulima kupitia mikutano yao ya mara kwa mara.

### Malengo ya muongozo huu

- Muongozo huu unalenga kuwapa wawezeshaji wa vikundi vya familia za wakulima katika eneo la mradi ujuzi wa hatua kwa hatua juu namna ya kuwasilisha mada ya jinsia kwa mfumo shirikishi.
- Muongozo ulilenga kuwaelekeza wafanyakazi wa taasisi na wawezeshaji wa vikundi juu ya masuala ya jinsia na kuwawezesha kuandaa mada za mafunzo kama ilivyoelekezwa.

Muongozo huu umeandaliwa kuwaongoza wawezeshaji wa vikundi vya familia za wakulima katika mchakato wa ufundishaji, kuwasaidia waweze kuelewa vizur, kupangilia, kuandaa na kusimamia usawa wa kijinsia na mafunzo ya jinsia katika ngazi ya familia na vikundi vya wakulima.

# 1.0 UTANGULIZI

Taasisi ya Kilimo Hai Tanzania (TOAM) ikishirikiana na Organic Denmark (OD) wameandaa muongozo wa mafunzo ya jinsia na vijana kupitia *program ya uwezeshaji wa familia za wakulima wadogo kupitia asisi za kidemokrasia, kilimo hai, upatikanaji wa masoko na upazaji sauti (ESFROMA)*. Lengo kuu la program hii ni kupunguza umasikini nan a kuongeza uhakika wa chakula kupitia kilimo hai na uwezeshaji wa wakulima wadogo ikiwa ni pamoja na wanawake na vijana Tanzania. Wanufaika wa program hii wakulima kutoka kata tano za wilaya ya chamwino mkoani Dodoma.

Lengo la tano la maendeleo endelevu 'Kuwepo na Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana Wote' ni moja mada muhimu katika program hii. Usawa wa kijinsia bado ni tatizo katika jamii za vijijini Uganda na Tanzania, pamoja na kwamba tafiti zinaonyesha tatizo la usawa wa kijinsia limepungua na kuongeza ufanisi katika Nyanja ya kilimo. Kwa mfano tafiti zimeonyesha kuwa, kwa kuwapa wakulima wa kike nchini Kenya pembejeo na elimu sawa na wakulima wa wakiume kungeongeza mavuno kwa asilimoa 20. Maeneo muhimu yanayohitaji usawa wa kijinsia ni pamoja na eneo la siasa na ndani ya familia; **Rejea Kiambatanisho IX.**

Maandalizi ya muongozo huu wa mafunzo ya ujumuishi wa kijinsia umehusisha mchakato wa ukusanyaji wa taarifa kuhusu masuala ya kijinsia na vijana ikiwa ni pamoja na kupitia machapisho na kushauliana na wataalam ili kuweza kuelewa dhana kamili.

## 1.2 Walengwa

Matumizi ya muongozo huu unalenga wafanyakazi wa taasisi ana wawezeshaji wa nje na wa ndani wa vikundi vya familia za wakulima ambao watafundishwa ili waende kufundisha wakulima katika vikundi vyao husika

## 1.3 Mbinu ya ufundishaji

Matumizi ya muongozo huu yamelenga kanuni zifuatazo za mafunzo ya watu wazima:

- Mafunzo yanalenga mtu binafsi.
- Kutimiza mahitaji ya haraka na kuwa shirikishi.
- Kijifunza ni kufanya (washiriki na muwezeshaji wanajifunza kwa pamoja)
- Muda uwepo kwa ajili ya mrejesho na marekebisho.
- Mazingira rafiki yawepo kati muwezeshaji na washiriki.

Popote inapowezekana, muunganiko wa mbinu mbalimbali kama maigizo, majadiliano kwa vikundi na michezo zinapaswa kutumiwa kama njia za kufikisha ujumbe kwa ufanisi Zaidi.

## 2.0 MUUNDO WA MUONGOZO

Muongozo umegawanyika katika moduli kuu tatu, kama zinavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

| Moduli | Yaliyomo | Malengo |
|---|---|---|
| **Moduli 1: Dhana na maana ya jinsi na jinsia** | • Maana ya dhana mbali mbali za jinsia<br>• Pengo la kijinsia na mifumo isiyo na usawa wa kijinsia<br>• Mifumo ya kisheria na kisiasa katika masuala ya jinsia ngazi ya familia. | Baada ya kumaliza mafunzo, washiriki wanapaswa wawe na uwezo wa:<br>• Kuelewa dhana na maana mbalimbali za masuala ya jinsia.<br>• Kutofautisha kati ya jinsi na jinsia.<br>• Kutafakari juu ya tofauti za jinsi na jinsia na athari zake kwa jamii.<br>• Kuwa mzoefu na mifumo ya sera inayohamasisha usawa wa kijinsia katika familia za wakulima wa kilimo hai na jamii kwa ujumla |

| Moduli | Yaliyomo | Malengo |
|---|---|---|
| **Module 2: uchambuzi wa jinsia** | • Elezea kanuni za uchambuzi wa jinsia<br>• Namna ya kutumia vifaa vya uchambuzi wa Kijinsia<br>• Kutafakari mgawanyiko wa kijinsia katika kazi, muundo wa kufanya maamuzi na upatikanaj/ ufikiaji na udhibiti wa rasilimali kwa jamii za wakulima.<br>• Jinsi ya kutathimini vigingi na vikwazo vinavyowakumba wanawake na wanaume. | • Elewa kanuni za uchambuzi wa jinsia..<br>• Kutumia vifaa vya uchambuzi wa jinsia<br>• Kutambua mahitaji mbalimbali na vipau mbele vya wanaume na wanawake katika jamii zao. |

| Moduli | Yaliyomo | Malengo |
|---|---|---|
| **Module 3: ujumuishaji wa usawa wa jinsia katika vikundi vya familia za wakulima** | • Dhana ya ujumuishi wa usawa wa kijinsia katika jamii za wakulima wa kilimo hai.<br>• Hatua na zana za kutathimini kiwango na uwezo wa familia za wakulima katika ujumuishaji wa masuala ya kijinsia. | • Kuelewa dhana ya ujumuishi wa usawa wa kijinsia kwa jamii ya vikundi vya familia za wakulima wa kilimo hai.<br>• Kujua mbinu za kimkakati za kuhusisha maswala ya kijinsia katika vikundi vya familia za wakulima wa kilimo hai.<br>• Kuandaa mipango ya kuzingatia suala la kijinsia katika vikundi vya wakulima wa kilimo hai. |

## 3.0 KUANDAA MAFUNZO YAKO

Muongozo huu umeandaliwa kuweza kutumiwa na wafanyakazi wa taasisi na wawezeshaji wa familia za wakulima wa kilimo hai kwa ngazi ya kikundi na familia. Unapoandaa mafunzo yako ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

- Mafunzo unayoandaa ni kwa ajili ya nani? Washiriki ni akina nani?
- Je kuna uhitaji wa haya mafunzo?
- Je mazingira ni rafiki kwa ajili ya kufanya mafunzo?
- Je mafunzo haya yatahusisha maeneo gani?
- Yapi ni matokeo ya mafunzo haya? Unalenga kufanikisha nini?
- Je zipo rasilimali za kutosha? Kama hazipo, wapi unaweza pata rasilimali za kukamilisha kazi hiyo.

## 4.0 MBINU KWA MUWEZESHAJI

Jinsia ni jambo la kibinafsi na kisiasa linalohusiana kwa ukaribu sana na mila na desturi ya washiriki hivyo mafunzo ya kijinsia yanaweza kuwa na changamoto na katika muktadha fulani ni kazi nyeti sana. Zifuatazo ni baadhi ya mbinu zinazoweza kumsaidia muwezeshaji anapojiandaa kufanya mafunzo ya jinsia:

- Jaribu kutengeneza mazingira rafiki ambapo kuna nafasi ya kutosha kwa ajili ya tathmini, uchambuzi na majadiliano ya wazi juu ya changamoto na fursa zinazohusiana na masuala ya jinsia na vijana. Epuka kufanya maamuzi kulingana na uzoefu wako binafsi na tamaduni zako.

- Himiza ushirikiano baina ya washiriki kwa kuwapa mazoezi ya pamoja, maswali na majibu na kazi za majadiliano.
- Andaa muda unaohitajika kwa ajili ya kufanya mafunzo kwa ufanisi Zaidi na uwe makini na muda kuhakikisha hutumii muda mwingi kwenye mada moja.
- Heshimu maoni ya washiriki na usiegemee upande wowote, toa ufafanuzi pale panapohitajika.
- Endelea kurekebisha mafunzo yako kwa kadiri washiriki wanavyotoa maoni yao.

# 5.0 VIAMBATANISHO MUHIMU

## 5.1 Kiambatanisho I: Muhtasari wa pendekezo la mafunzo

| **Muhtasari wa pendekezo la mafunzo** |
|---|
| Mwelekeo mzima wa mafunzo<br>Ujumuishi wa masuala ya jinsia na vijana katika vikundi vya wanafamilia wa kilimo hai. |
| **Mantiki ya mafunzo** / *kwa nini kuna uhitaji wa haya mafunzo*<br><br>Kiwango kidogo cha uelewa na ujuzi kwenye masuala ya jinsia baina ya wanafamilia na wanakikundi wa kilimo hai. |
| **Lengo la mafunzo** /*unataka kufanikisha baada ya mafunzo kwa ujumla*<br><br>**Lengo kuu:** kuhamasisha kaya zinazolengwa (vijana na wanawake) kushiriki katika uzalishaji wa kilimo hai na nafasi za uongozi katika jamii.<br><br>**Lengo mahususi:** ushusishaji wa masuala ya jinsia na umri kwa jamii ya wakulima wa kilimo hai. |
| **Mbinu** : shirikishi, kazi za vikundi, maswali na majibu. |

**Mada zilizopendekezwa.**

**Moduli 1**: Nini maana ya jinsia: ufafanuzi wa dhana za msingi za jinsia.

*Dhana za jinsisa na maana zake.*

*Pengo la jinsia na mifumo isiyo na usawa wa kijinsia*

*Mifumo ya kisheria na kisiasa katika masuala ya usawa wajinsia*

**Moduli 2:** Fafanua dhana muhimu kupitia uchambuzi wa jinsia.

Mambo muhimu katika uchambuzi wa jinsia

- Kanuni za uchambuzi wa jinsia.
- Utangulizi na utumiaji wa zana za uchambuzi wa jinsia.
- Upatikanaji/Ufikiaji na udhibiti wa rasilimali, mali na faida.
- Mahitaji ya kijinsia ya msingi yay a kimkakati
- Mgawanyo wa kazi

**Moduli 3**: Ujumuishaji wa usawa wa kijinsia katika vikundi vya familia za wakulima

- Dhana ya uhusishaji wa usawa wa jinsia katika jamii za wakulima wa kilimo hai.
- Hatua na zana za kutathimini kiwango na uwezo wa familia za wakulima katika ujumuishaji wa usawa wa jinsia.

## 5.2 Kiambatanisho II: Ajenda ya muwezeshaji

| Muda na mada inayowasilishwa | Maelezo |
|---|---|
| Kufungua na kukaribisha washiriki<br>Kupitia kwa ufupi ajenda na malengo ya mafunzo | |
| Moduli 1: dhana ya jinsia | Mbinu itakayotumika |
| Lengo: washiriki waelewe dhana ya jinsia na maana zake<br><br>Matokeo ya kipindi: Washiriki wameelewa dhana nzima ya jinsia na maana zake. | 1. Katika makundi (wanawake wanaume na vijana) washiriki wajadili na kuandaa igizo kuhusu uelewa wao wa usawa wa jinsia.<br><br>2. Uwasilishaji wa kazi za vikundi<br><br>3.Ufafanuzi wa muwezeshaji kwenye maana mbalimbali za jinsia. |
| Moduli 2: Uchambuzi wa jinsia<br>Lengo ni washirika waje na masuala ya kijinsia na changamoto ambazo mafunzo yatazifanyia kazi.<br><br>Matokeo ya kipindi:<br><br>Mambo yaliyopewa kipaumbele yaweze kushughulikiwa na mradi | 1. Muwezeshaji kuwaongoza washiriki kuweka kipau mbele kwenye masuala ya kijinsia yanayotakiwa kushughuikiwa na mradi.<br><br>2. Uwasilishaji wa kazi za vikundi na majadiliano. |

| Muda na mada inayowasilishwa | Maelezo |
|---|---|
| Moduli 3: Ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika vikundi vya familia za wakulima | Lengo: washiriki waje na mabadiliko wanayotamani kuayaona baada ya kushughulikiwa kwa mambo yaliyopewa kipau mbele hapo juu.<br><br>Matokeo ya kipindi: mkakati wa jinsia wa kushughulikia masuala ya kijinsia<br><br>1. Kupitia vikundi, washiriki wajadili maboresho wanayotaka kuyaona<br>2. Washiriki wajadili maengo na mikakati itakayojadiliwa tena kwa pamoja wakati wa uwasilishaji.<br>3.Washiriki wajadili shughuli/mbinu za kuwawezesha kufikiam malengo hayo<br>4. Uwasilishaji wa kazi wa vikundi na majadiliano ya pamoja.<br>5. Ufafanuz wa muwezeshaji kwenye malengo na mbinu zilizopendekezwa. |

## 5.3 Kiambatanisho III: Programu ya mafunzo

| SIKU YA KWANZA | |
|---|---|
| **Muda** | **Mada** |
| **9:00 – 10:00** | Usajili na kupata matarajio ya washiriki kuhusu mafunzo hayo |
| **10:00 -10:30** | **Moduli 1**<br>Utambulisho wa washiriki na muhtasari wa mafunzo |
| **10:30-11:15** | **MAPUMZIKO YA CHAI** |
| **11:15– 12:30** | Utangulizi wa dhana ya jinsia na maana zake ( majadiliano na uwasilishaji) |
| **12:30-13:00** | Pengo la jinsia na mifumo isiyo na usawa wa kijinsia |
| **13:00– 14:00** | **CHAKULA CHA MCHANA** |
| **14:00-15:00** | Mifumo ya kusheria na kisiasa ya usawa wa jinsia. |
| **15:00-16:00** | **Moduli 2**<br>Utangulizi wa uchambuzi wa jinsia, kushirikishana kanuni za uchambuzi wa jinsia. |
| **16:00-16:15** | Kufunga kwa siku ya kwanza |
| **SIKU YA PILI** | |
| **9:00-9:30** | Usajili wa washiriki |
| **9:30-10:00** | Tafakari ya siku ya 1 (walichojifunza na uzoefu) |
| **10:00-10:30** | Utangulizi wa uchambuzi wa jinsia |
| **10:30-11:15** | **MAPUMZIKO YA CHAI** |
| **11:15-12:00** | Utangulizi wa zana za uchambuzi wa jinsia na matumizi yake. (uwasilishaji na majadiliano) |
| **12:00-13:15** | Kufanya tathimini ya mgawanyo wa kazi, mifumo ya kimaamuzi na udhibiti wa rasilimali kwa jamii ya wakulima (kazi ya kikundi na kushirikishana uzoefu) |
| **13:15 -14:15** | **CHAKULA CHA MCHANA** |
| **14:15 - 15:15** | Uwasilishaji wa kazi za kikundi. |
| **15:15-16:00** | Kufanya tathimini ya changamoto wanazozipata wanaume na wanawake (majadiliano ya pamoja na uwasilishaji) |
| **16:00-16:15** | Kufunga kwa siku ya pili |

| SIKU YA TATU | |
|---|---|
| **9:00-9:30** | Usajili wa washiriki |
| **9:30-10:00** | Tafakari ya siku ya 1 (walichojifunza na uzoefu) |
| **10:00- 10:45** | **MAPUMZIKO YA CHAI** |
| **10:45- 11:45** | Dhana ya ujumuishaji wamasuala ya jinsia katika vikundi vya familia za wakulima wa kilimo hai (majadiliano na uwasilishaji) |
| **11:45-13:00** | Utangulizi kuhusu hatua na zana za kutathimini kiwango na uwezo wa vikundi vya familia za wakulima wa kilimo hai katika masuala ya jinsia. |
| **13:00 – 14:00** | **CHAKULA CHA MCHANA** |
| **14:00-15:15** | Kazi ya kikundi na uwasilishaji<br>*mbinu zilizopo za kutathimini kiwango na uwezo wa kuhusisha musuala ya kijinsia katika jamii na wakulima wa kilimo hai. |
| **15:15-16:00** | Makubaliano<br>*majadiliano ya pamoja na kuandaa mpango kazi wa kuhusisha masuala ya jinsia katika vikundi vya familia za kilimo hai na jamii. |
| **16:00-16:10** | MWISHO WA MAFUNZO (maneno ya kufunga na kutawanyika) |

## 5.4 Kiambatanisho IV: Zana ya uchambuzi wa jinsia, uwezo wa kufikia na kudhibiti rasilimali kwa ngazi ya familia na siasa.

| | **kufikia (nani)** | | | **Kudhibiti (nani mwenye mamlaka)** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Rasilimali** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Vijana** | **Wanaume** | **Wanawake** | **Vijana** |
| Ardhi | | | | | | |
| Zana | | | | | | |
| Nguvu kazi | | | | | | |
| Kipato cha familia | | | | | | |
| Elimu/mafunzo | | | | | | |
| **Ngazi ya siasa** | | | | | | |
| Uongozi(uwakilishi ngazi ya uongozi) | | | | | | |
| Kufanya maamuzi | | | | | | |
| Mengine | | | | | | |

## 5.5 Kiambatanisho V: Tathimini ya mahitaji ya kijinsia ya msingi

Tafadhali jaza maswali yafuatayo. Majibu yako yatatusaidia kujua vipaumbele na uhitaji wenu katika mafunzo ya jinsia.

1. Jina: (sio lazima) ……………………………………………………….
2. Nafasi yako: (sio lazima) ………………………………………………..

3.Umewahi kushiriki katika mafunzo yanayohusu masuala ya kijinsia?**Ndio/ Hapana**. (kama ndio elezea ni wapi na vitu ulivyojifunza)

4. Unaelewa nini kuhusu neno jinsia?
5. Je tayari umeshahusisha masuala ya kijinsia katika mipango kazi yako? Kwa namna ipi?
6. Umewahi kukutana na changamoto yoyote wakati unahusisha masuala ya kijinsia katika kazi zako? Kama ndio ni changamoto gani?
7. Yapi ni malengo muhimu mawili ambayo unalenga kuyafanikisha kwa kuhudhuria mafunzo haya?

8. Tafadhali jitathimini kiwango cha uelewa wako kwa sasa katika mada zifuatazo: (1- Sielewi mada kabisa…..5 Nimeelewa mada vizuri kabisa)

- Uchambuzi wa kijinsia na dhana ya jinsia kwa ujumla
- Uingizwaji wa masuala ya jinsia, maana yake nini.
- Uingizwaji wa masuala ya kijinsia katika vikundi vya familia za wakulima wa kilimo hai.

## 5.6 Kiambatanisho VI: Masuala ya jinsia na mfumo wa kimkakati.

Mfumo huu utamsaidia muwezeshaji na washiriki kuweka vipaumbele na kuainisha mambo ya kijinsia yanayohitaji kufanyiwa kazi na mikakati ya kuyatatua.

| | |
|---|---|
| **Kipaumbele 1** | …………………………………….. |
| **Maelezo** | ……………………………….. |
| **Mikakati** | • ………………………..<br>• ………………………..<br>• ……………………….. |
| **Shughuli** | • .........................................<br>• .........................................<br>• .......................................... |
| **Viashiria** | Ufuatiliaji wa utendaji: Anzisha kwa kila shughuli, wanaume wangapi, wanawake na vijana watashiriki.<br>1. ……………………………………<br>2. ……………………………………<br>3. …………………………………….. |

## 5.7 Kiambatanisho VII: Muongozo wa tathimini na maswali baada ya mafunzo.

Tafadhali tumia dakika zako chache na zingatia maswali yafuatayo kutusaidia kufanya tathimini ya mafunzo haya ili kuweza kuyaboresha kipindi kijacho. Onyesha kuridhika kwako kwa kutumia namba 1-5. (1 sijaridhika kabisa….5-nimeridhika kabisa)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Mada za kufundisha | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Kazi za vikundi | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Uwasilishaji/majadiliano ya pamoja | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| Mbinu na ujuzi wa kufundisha | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

Je mafunzo yamefikia matarajio yako? Ndio/ hapana

Kama mafunzo haya hayafikia matarajio yako tafadhali tuambie ni matarajio gani ambayo hayakufikiwa.

Tafadhali ainisha vitu ulivyoviona vinakufaa kwenye mafunzo haya.

Tafadhali ainisha vitu ulivyoviona havikufai kwenye mafunzo haya.

Elezea ni kwa nini

Unatathimini vipi kiwango cha uelewa wako sasa baada ya mafunzo kwenye mada zifuatazo (ainisha mada kama zile za tathimini ya kabla ya mafunzo)

(5 – nimeelewa mada vizuri kabisa ….. 1 – Sijaelewa mada kabisa)

- Uchambuzi wa kijinsia na dhana ya jinsia kwa ujumla
- Uingizwaji wa masuala ya jinsia, maana yake nini.
- Uingizwaji wa masuala ya kijinsia katika vikundi vya familia za wakulima wa kilimo hai

Kuna kingine chochote ungependa kutushirikisha?

Asante kwa muda wako!

## 5.8 Kiambanisho VIII: mbinu za kuunda makundi

Ili kuweza kupata makundi kwa ajili ya kurahisisha kujifunza, jaribu kutumia njia tofauti za kuwagawa washirika katika makundi tofauti. Zifuatazo ni baadhi ya mbinu zinazoweza kutumika kutengeneza makundi:

**Hatua 1**: Waambie washirika wapange mstari kulingana na urefu wao (kuanzia mfupi hadi mrefu), au kulingana na herufi za majina yao (kuanzia A hadi Z)

**Hatua 2**: Tumia mstari kama msingi wa kuunda makundi kwa kukusanya washirika wa kwanza wachache katika kundi moja au wagawanye kwa kumuweka mshirika wa kwanza katika kundi la kwanza mshirika wa pili katika kundi la pili ..n.k

Njia nyingine ya kuunda makundi ni kuhusisha kazi hii na zoezi dogo la viungo:

**Hatua 1**: waambie washiriki watembee kuzunguka chumba (unaweza kuwaonyesha wazunguke kwa namna gani wanapaswa kuzunguka-kwa kutembea kukimbia au kucheza).

**Hatua 2**: tumia mpangilio huu kama msingi, wagawanye kwenye makundi kulingana na walivokaa karibu.

## 5.9 Kiambatanisho IX: Mpangilio na vifaa

| Idadi ya Wakufunzi (Wafanyakazi wa TOAM) | Idadi ya Washiriki (wawezeshaji wa ndani na nje-FFLG) | | Eneo la mafunzo | Nakala za mwongozo na vifaa vingine | Gharama |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | **M** | **F** | Wilaya ya Chamwino | Nakala 110 za mwongozo wa mafunzo, Karatasi mgeuzo, Kalamu alama za kuandikia , na vifaa vingine vinavyohusika | *Gharama za usafiri<br>*Gharama za chakula na malazi<br>*Gharama za ukumbi<br>*Dharura |
| | 52 | 58 | | | |

**Tanzania Organic Agriculture Movement (TOAM)**
Ghorofa ya tatu I Jengo la Skyway Building I Mtaa wa Ohio na Sokoine Drive I Dar Es Salaam.
S.L.P 70089 I Simu: +255 710 267652/0756950273/
Barua Pepe: toam@kilimohai.org/info@kilimohai.org